MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 2 TOLEO 2

SEPTEMBA 9, 2008

KIJARIDA CHA BURE— UKISHASOMA MPE MWINGINE—USIBANIE!

"TUNALAANI MAUAJI YA ALBINO" - EU



Mtoto Albino

Na. Fred Katunzi



Bunge la nchi za Ulaya limelaani vikali mauaji ya Watanzania wenye upungufu wa chembe zinazotengeneza rangi mwilini waitwao Maalbino. Kauli hiyo imetolewa na Bunge la Ulaya wiki iliyopita mara baada ya kikao chake mwishoni mwa juma lililopita

Katika azimio lake la kulaani mauaji ya Albino nchini, JU (Jumuiya ya Ulaya) imesema kuwa imeendelea kushtushwa na "taarifa kuwa kuna mauaji ya Albino nchini Tanzania". Pamoja na kushtushwa huko Bunge hilo limesema linatiwa moyo na hatua kadhaa ambazo zimechukuliwa na vyombo mbalimbali vya serikali katika kupambana na mauaji hayo ambayo msingi wake ni imani za kishirikina.

Taarifa mbalimbali zinaonesha ndani ya miezi michache iliyopita zaidi ya Maalbino 25 wameuawa sehemu mbalimbali nchini kutokana na tamaa ya utajiri wa haraka haraka.

Ualbino hutokana na upungufu wa rangi mwilini

Mauaji haya yanaambatana na kukatwa viungo vya marehemu kwa matumizi ambayo wahalifu hao wanaamini kuwa yatawaletea bahati katika maisha au biashara zao.

Pamoja na kutambua juhudi hizo za kukabiliana na wimbi la mauaji hayo Bunge la JU limetoa wito kwa serikali "vyombo vyake, serikali za mitaa, na taasisi za kiraia kushiriki kuhakikisha kuwa vinawalinda maalbino wote." Zaidi ya yote linawataka "kuchukua hatua mara moja kuielimisha jamii kuhusu masuala ya Ualbino na juhudi hizo zielekezwe zaidi maeneo ya vijijini ambapo watu wengi hawajaelimika na wanaamini mambo ya kichawi".

Jamii hii ya watu wenye mapungufu hayo ya rangi kwa muda mrefu walikuwa wanajulikana kama "zeruzeru". Hata hivyo kutokana na jina hilo jamii nyingi nchini wamekuwa wakiwaona wenye ualbino kama kioja na hivyo jina la "zeruzeru" linaonekana kuwa ni la kunyanyapaa na limeacha kutumiwa na badala yake jina la Albino ndilo linatumika.

Watu wasioelewa bailojia au elimu viumbe wamekuwa wakitumia kutojua hali ya inaendelea) kama sababu ya kisingizio cha kuwabagua, kuwatenga, kuwatesa **(inaendelea)**



Benjamin. G. Mwalukasa
Mhariri

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Jumanne**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.**
- **Ni kijarida chako!**
- **Haki zote za kuchapa zimeruhusiwa!**

HOJA YA MWANAKIJIJI— NAPE USIPIGE MAGOTI!

Nape Nnauye hakujua kuwa alikuwa ameshika makali wakati "Dr". Nchimbi na wenzake wameshika mpini.

Uamuzi wa Baraza kuu la Umoja wa Vijana wa kumvua uanachama wa UVCCM kwa madai ya utovu wa nidhamu ni ishara na ujumbe wa wazi kwa vijana wengine wote ndani ya chama hicho ambao wana fikiria kufichua vitendo vya kifisadi "nje ya taratibu za chama" kuwa wazo hilo life.

Ujumbe wa uamuzi huu dhidi ya Nape uliotolewa siku ya Jumapili ni kama onyo kwa UVCCM kama wale wa Tanga na sehemu nyingine ambao wanathubutu kutoa changamoto kwa vigogo wa Chama hicho kuhusu ufisadi.

Uzuri wa roho ya ujana ni kukataa kuburuzwa na kushinikizwa. Tunachosubiri kuona sasa ni jinsi gani wana UVCCM nchini watakubali maamuzi haya na kama wote watafyata mikia yao na kuogopa jinamizi la nidhamu ya Chama.

TUNASEMA, Nape asikatishwe tamaa kwani hii ni gharama tu ya maamuzi ya kutetea nchi yake. Afanye kama alivyofanya Zitto; asipige magoti mbele ya mafisadi!!

Ndani ya Toleo Hili

EU na Mauaji ya Albino	1
Hoja ya Mwanakijiji	1
Vigogo wa Ufisadi —1	2
Mauaji ya Albino	2
Wanaoepnda kubishana	3
Jessy: Maadili ya Picha	3
Picha, Katuni na Maoni	4

HABARI MBALIMBALI

SAILETH VITHLANI— KIGOGO WA UFISADI

Na. Mahmoud Rashid



Wiki hii tunaanza mfululizo wa "vigogo wa ufisadi" Tanzania ambao ni kiini cha matatizo na kina cha kuenea vitendo vya rushwa kubwa nchini.

Tutawaangalia kwa majina vigog hawa na yale ambayo wamedaiwa kuyafanya. Ni lengo letu madai yetu dhidi yao yatasababisha vyombo vya sheria kuchukua hatua za uchunguzi na hatimaye kuwafungulia mashtaka yanayostahili.

Mmojawapo wa watu ambao wameiletea hasara nchi yetu ni raia wa Uingereza aitwaye Saileth Vithlani (pichani).


Bw. Vithlani anakabiliwa na kesi namba 1474 ya mwaka 2007 katika mahakama hiyo ya Kisutu baada ya kudaiwa kusema uongo.

Bw. Vithlani (ambaye aliwahi kuwa raia wa Tanzania) ndiye aliyehusika na udalali wa bidhaa nyingi kwa serikali yetu nyingi (kama siyo zote) zikiwa katika bei ya kulangua.

Siku chache kabla ya kufunguliwa kesi katika Mahakama ya Kisutu Bw. Vithlani alitoweka na kwenda kuishi Geneva Uswisi ambako anaishi kama mtu huru licha ya kujua aliko na kutoomba msaada wa Polisi wa Uswisi kumkamata na kumrudisha nchini.

Anakabiliwa na kesi Na. 1474 ya mwaka

Bw. Vithlani ndiye kigogo wa Rada ambaye inadaiwa alikatiwa "mshiko" wa karibu bilioni 21 za Kitanzania ambazo licha ya yeye mwenyewe kukana anatuhumiwa kuzigawa kwa vigogo mbalim-



Saileth Vithlani (Shilu)

bali wa serikali miongoni mwao akiwa ni aliyewahi kuwa Mwanasheria Mkuu na baadaye Waziri wa Miundo Mbingu Bw. Andrew Chenge (Mzee wa Vijisenti".

Bw. Vithlani (pamoja na mshirika wake tutakayemwangalia wiki ijayo) ameshiriki katika miradi mbalimbali ikiwemo uuzaji wa ndege ya kisasa ya Rais, Boti za Polisi, Malori ya IVECO na helikopta za Bell kwa JWTZ.

Inadaiwa kuwa Bw. Vithlani katika biashara zake na serikali ameiiuzia Tanzania vitu vyenye thamani ya zaidi ya dola milioni 245 (Karibu bilioni 250) lakini hiyo ikiwa bei ya kulangua kwa karibu asilimia 45!

Kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali Bw. Vithlani amejikita kwenye urafiki wa karibu na vigogo mbalimbali wa kisiasa (ambao tutawataja matoleo yajayo) na hivyo kuwa vigumu kweli kumfikisha mahakamani yeye maswahiba wake.

Juhudi zote za kumpata ili ajibu tuhuma dhidi yake zimeshindikana.

(Itaendelea wiki ijayo)

MAUAJI YA ALBINO (KUTOKA 1)

na kuwachukulia kama alama ya mkosi.

Neno Albino linatokana na lugha ya Kilatini lenye maana ya 'weupe' kwani watu wenye upungufu huo wa rangi wanakuwa na rangi nyeupe zaidi kuanzia nywele, ngozi na wengine hata macho.



Tausi mwenye Ualbino

Hata hivyo maendeleo ya sayansi na teknolojia yanaonesha kuwa matatizo ya upungufu wa rangi siyo jambo la Watanzania tu bali jamii zote za binadamu na tangu enzi na enzi kumekuwapo na watu wenye matatizo hayo. Zaidi ya yote wataalamu wanaonesha kuwa Ualbino ni hali ambayo inawakuta karibu viumbe vyote kuanzia binadamu, wanyama wa pori, wafugwao na hata samaki na ndege kama picha ya tausi albino inavyoonesha hapo kushoto.

Kutokana na ukweli huo wa kisayansi ni utapeli na ulaghai mkubwa kuhusisha mafanikio ya kibiashara na mauaji ya binadamu ambayo msingi wake ni imani za kichawi. Kama Ualbino ni dawa basi wenye tamaa waende kutafuta samaki na ndege albino na kuwaacha binadamu.

Cheche linatoa wito kwa Watanzania wote kupinga kwa nguvu zote udhalilishaji huu wa ndugu na jamaa zetu na zaidi ya yote kutoa elimu ya matatizo haya, kuwashikilisha katika shughuli mbalimbali na kuwapa nafasi sawa katika kila hali.

Zaidi ya yote, tunatoa wito kwa Serikali na Wafadhili, taasisi za dini, na vikundi vya kiraia kutoa misaada ya miwani, dawa za ngozi, kofia na vifaa mbalimbali ambavyo vitawasaidia Maalbino kuishi maisha ya kawaida zaidi. Tunaamini kama Taifa tunauwezo wa kushinda uovu huu kwenye jamii yetu.

UKIMALIZA KUSOMA MPATIE MWINGINE BURE!

NGUVU ZA HOJA

TAIFA LA WANAOPENDA KUBISHANA

Na. B. Mwalukasa

Watanzania tuna mazoea fulani mabaya. Mazoea ambayo ni vigumu mno kuachana nayo kiasi kwamba tumeyakubali kama vile ni hulka yetu vile. Mazoea ya kupenda kuzungumza bila kufikia kikomo na hatimaye kutenda. Tumejenga mazoea ya kubishana hadi tunapokaribia kufika mwisho tunaamua tuanze kubishana juu ya mabishano mengine.

Mtindo huu ni wa kijiweni ambapo mabishano ya leo yanaendelea kesho na ya kesho yataendelea keshokutwa. Kama huamini angalia mahali ulipo ni lini mmebishana au kujadiliana juu ya jambo lolote jipya zaidi ya mwendelezo wa lile lililopita?

Kilele cha tabia hii kinaonekana katika matendo ya viongozi wetu na taasisi mbalimbali za kitaifa ambazo zinapoteza muda mrefu kuzungumza kiasi kwamba hata inapofika wakati wa kuamua kutenda wanajikuta wanaanza kuzungumza tena. Mazungumzo yetu ya kitaifa hayakomi na maamuzi hayafanyiki isipokuwa ya kuamua kuzungumza zaidi.



Angalia suala la Richmond kwa mfano. Tumekubaliana kuwa tumetapeliwa, tumekubaliana kuwa kuna uzembe umefanyika, na tumekubaliana kuna watu ambao hawakuwajibika. Sasa katika nchi ya watu wanaotenda leo hii kuna watu wangekuwa wameshafikishwa mahakamani, fedha zilizolipwa kinyume na sheria kurudishwa na waliohusika wote kuwajibishwa.

Siyo Tanzania! Baada ya uchunguzi wa Kamati Teule na mazungumzo mazito Bungeni tulitarajia vitendo vingefuata. Cha kushangaza Waziri Mkuu amekuja na mazungumzo mengi ambapo watu wanatakiwa waandike maelezo ambayo sitoshangaa yatajibiwa kwa barua nyingine zitakazohitaji ufafanuzi zaidi. Baadaye mazungumzo hayo yataletwa Bungeni na kuzaa mjadala mwingine ambapo itaamuliwa serikali ifanye mazungumzo na wahusika ili kuona kama wanaweza kuachia ngazi bila kuishtaki serikali.

Tunaweza kuangalia suala la Muafaka wa Zanzibar mambo ni hivyo hivyo. Wameanza kuzungumza kuanzia 1995! Na hili la "nchi si nchi" litachukua muongo mzima. Tunapenda kuzugumza mno kuliko kutenda.

Ipo mifano mingine kama sakata la waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika ya Mashiriki iliyovunjika ambao majadiliano nayo yameendelea kwa karibu miaka thelathini sasa.

Ni lazima tuchoke kuzungumza na tufikie mahalai tufanye maamuzi. Vingine tutajikuta tunazungumza hadi tunasahau tulichokuwa tunazungumzia mwanzoni na mwisho kufuta kesi zenyewe na kuwaacha mafisadi wakiendelea kutamba.

Ni lazima tujifunze kufika mwisho wa majadiliano kwa kufanya vitendo na kuchukua hatua. Majadiliano lazima yafikie mahali yalete maamuzi, ambayo yataonekana kwa vitendo. Swali ni panya gani atamfunga paka kengele?

MAADILI YA PICHA MTANDAONI

Na. Jessica Leonard Fundi

Wiki iliyopita rafiki yangu mmoja aliniambia jambo ambalo limenifanya nifikirie. Rafiki yetu mwingine (tulisoma pamoja) amejikuta anapigiwa simu nyingi kutoka kila kona baada ya picha yake kuwekwa mtandaoni na yeye kudaiwa kuwa ni malaya wa kutupwa.

Dada huyo ambaye ni mke wa mtu na ni mfanyakazi katika idara nyeti tu amekaribia kujidhuru maisha yake hasa baada ya mambo ya ujana wakati akiwa chuoni kuanikwa kwenye mtandao wa intaneti.

Tulipoamua kulifuatilia suala hilo tumekuta siyo yeye tu bali watu wengi ambao ni wake na waume za watu au mabinti na watoto wa watu wakiandikwa kwenye mtandao ambapo baadhi ya watu wanaamua kuwatukana, kuwazulia uongo, na zaidi ya yote kuwafanyia kile ambacho kinaitwa kama "cyber bulling".
Ubabe wa kwenye mtandao (cyber bulling) kwenye baadhi ya nchi umeanza kuandikwa kwenye sheria kwani una lengo la kumuonea mtu ambaye hana uwezo wa kujitetea na hasa pale mtu anayemuonea akiwa amejificha nyuma ya kompyuta. Vitendo hivi vya kibabe vinahusu maisha ya



mapenzi, utumishi, ndoa, urafiki n.k na vinaendena na madai ya kumdhalilisha mtu na imefikia mahali picha za watu zinawekwa mtandaoni aidha na waliowahi kuwa marafiki au zinachotwa kutoka kwenye tovuti mbalimbali rasmi.

Mstari ulioanza kuvukwa ni pale mmoja wa Mawaziri wa serikali ya Rais Kikwete alipoandikwa mambo yake ya ndani na ya chumbani.

Kuna wale wanaoona kuwa viongozi wa umma hawana maisha binafsi tena na lolote wanalofanya ni "fair game" na hivyo siri za Marais, Mawaziri, Wabunge, Wachungaji, Mashehe n.k vyote ni vya kuwekwa kwenye mtandao wa intaneti.

Soma bure

Hilo linaweza kukubalika kwenye nchi nyingine.

Lakini tunapofikia kuanza kuwaandika watu ambao si watumishi wa umma, si waomba kura wa nchi hii basi tunavuka mpaka wa uhuru wa maoni na kufikia mahali pa ubabe wenye lengo la kuvuruga mahusiano ya watu na kuhatarisha maisha yao.

Ni lazima tutafute njia muafaka ya kukabiliana na ubabe huu wa mtandaoni.

MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...


Picha ya Wiki



Will Smith alipokutana na Rais Aman Karume

KATUNI ZA WIKI







KUTOKA KWENYE MTANDAO

Hatua hii (kumvua uanachama Nape) ni fundisho kwa wana UVCCM wote wanaotaka kudiriki kuhoji kwa nini wazee wanaopaswa kuwa mfano kwao wanaifisadi jumuia yao. Vijana kuweni na adabu, acheni mambo ya kikubwa—**Kijana**

Sasa ni wakati wa Nape kujipanga upya na kutafuta nafasi zingine za uongozi ziko nyingi sana, sasa ni kazi ya CC kudeal na uhuni wa jengo la vijana—**FMES**

Sasa tumepata uthibitisho rasmi kwamba kweli CCM ni Chama Cha Mafisadi na hawastahili kabisa kuwepo madarakani kwa kuwa matatizo yetu mengi Tanzania yanasababishwa na CCM. CCM ni kikwazo kikubwa cha maendeleo ya Tanzania.—**Bubu Ataka Kusema**

Nape unasubiri nini kuihama hiyo CCM! Kajiunge na akina Zitto na wengine. Hao wazee chochote watakachokuambia, watakuwa wanafiki tu! Wewe jina huko limechafuka na haliwezi kusafishika! Maadam wewe ni mwanasiasa, hamia upinzani— **Haki.Tupu**

Hii nadhani ni fundisho kwa vijana wengine na wapenda nchi yao. Tusisubili wakati wa kuomba kura ndiyo tupambane na fisadi, hapo unakuwa si mpambanaji bali unafiki kiasi fulani au unatafuta njia ya kukutangaza si vita endelevu.—**Ukuni Mkavu**

Nape kafanya kosa moja kubwa kimkakati, ambalo nadhani ndilo liliyomcost nafasi zake kwenye Chama chake. Alianza vibaya sana kwa kujaribu kumnyang'anya fisadi upanga huku akimwabia waziwazi kuwa ukiniachia upanga huu nitautumia kukukata shingo, wakati fisadi huyo bado kashika mpini wa ule upanga.— **Kichuguu**

UVCCM ni taasisi kubwa na haitegemewi kukosa mwendawazimu kama ilivyo mahala pengine popote penye watu wengi, kinachotakiwa ni kuwashughulikia na kuwarudisha katika mstari. Uongozi hauji kwa kujivuna wala kulumbana na wakubwa walio juu kinachotakiwa ni kuwa na staha na kufuata maadili ya chama— **"Dr". E. Nchimbi**

Cheche za Fikra

Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi

Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha, maoni, habari, na ushauri

Tuandikie: **Mhariri@klhnews.com**

Tembelea: **http://www.klhnews.com**

***Kanusho:** Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.*